

Umuhimu wa Maarifa ya الْوَقْفُ وَالْإِبْتِدَاءُ Al-Waqfu Wal-Ibtidaai - Kisimamo Na Kianzio:

Kusimama na kuanza ni katika sehemu muhimu kabisa katika fani ya sayansi ya Tajwiyd, ambayo msomaji anatakiwa aishughulikie ipasavyo ili aweze kutambua mahali panapofaa kusimama na pasipofaa na atambue mahali panapopasa kuanzia ili asiharibu kauli kwa kukata maneno yaliyotangulia na yanayotakiwa kuungana kwani atakuwa amepoteza maana iliyokusudiwa.

Imepokewa kuwa 'Aliy bin Abi Twaalib (رضي الله عنه) aliulizwa kuhusiana na kauli yake Allaah:

﴿ وَرَتِّلِ الْقُرْآنَ تَرْتِيلاً ﴾

“... na soma Qur-aani kwa tartiylaa [kisomo cha utaratibu upasao]”¹

Alijibu:

هُوَ تَجْوِيدُ الْحُرُوفِ وَمَعْرِفَةُ الْوُقُوفِ

“Ni kuisoma Qur-aan kwa ujuzi wa kutamka herufi ipasavyo na kuwa na ujuzi wa hukmu za kusimama”

Alikuja mtu kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akahutubia mbele ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema:

"مَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ رَشَدَ وَمَنْ يَعْصِيهِمَا (وقف ثم قال:) فَقَدْ غَوَى". فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ((قُمْ أَوْ اذْهَبْ بِئْسَ الْخَطِيبُ أَنْتَ))

“Atakayemtii Allaah na Mtume Wake ameongoka na atakayewaasi (akasita kisha akaendelea.): amepotoka”: Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم) ((Simama! [au] Nenda! Khatibu mbaya uliyoje wewe))²

Kusimama katika: “Na atakayewaasi” lilileta maana kwamba atakayemtii Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume (صلى الله عليه وسلم) na atakayewasi wote watakuwa ni wenye kuongoka. Alipaswa aendelee kauli mpaka mwisho bila ya kusita au

¹Al-Muz-zammil (73 : 4)

²Abu Daawud

asimame baada ya 'ameongoka' kisha aendelee yanayofuatia hapo ingeliondosha utata huo.³

Kosa la kutokusimama katika neno lilitokea pia zama za Maswahaba⁴

Ingawa fani ya **الْوَقْفُ وَالْإِبْتِدَاءُ (Al-Waqfu Wal-Ibtidaai)** inahitaji ufahamu wa lugha ya Kiarabu ili kufahamu maana ya maneno ya Qur-aan, lakini ni neema kwamba Maulamaa wa Qur-aan wamesahilisha jambo hili kwa kubainisha hukmu hii ya **الْوَقْفُ وَالْإِبْتِدَاءُ (Al-Waqfu Wal-Ibtidaai)** kiasi fulani kwa kuweka alama mbali mbali za kusimama na kutokusimama katika misahafu.

³ Na katika riwaaya iliyorekodiwa na Muslim **impokewa toka kwa 'Adiyy bin Haatim (رضي الله عنه) kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliendelea kusema: ((...bali sema: Na atakayemuasi Allaah na Mtume Wake))**. Wanachuoni wamefafanua Hadiyth hii kwamba huyo mtu amemsawazisha Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kuwaunganisha katika *dhwamiyr* (kiwakilishi nomino). Alipaswa atenganishe kumtaja Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa kusema **"na atakayemuasi Allaah na Mtume Wake basi amepotoka"**.

⁴ Abu Bakr (رضي الله عنه) alipokuwa sokoni siku moja akitafuta kitu kadhaa. Alipomuuliza mwenye duka kama anacho hicho kitu dukani kwake, alimjibu: **"لا يرحمك الله (Laa Yarhamuka-Allaah!)"**. Kwa maana: "Hapana Allaah Asikurehemu". Imefahamika hivyo kwa sababu hakusimama katika neno لا ambalo pindi angelisimama ndipo ingeleta maana aliyokusudia yaani alikusudia kusema: **"Hapana sina!. Allaah Akurehemu"**. Ndipo Abu Bakr (رضي الله عنه) almwambia: **"Ingelikuwa bora kama ungelisimama baada ya 'laa' (hapana) kisha uendelee 'Allaah Akurehemu"**